

٢٠ شعبان ١٤٤٠ هـ  
٢٦ إبريل ٢٠١٩ م

جمهورية مصر العربية  
وزارة الأوقاف

(١)

Mambo yanayozijenga Nchi.  
Prof. Ayman Alasar.

Sifa zote njema ni zake mwenyezi Mungu Mtukufu Mola wa  
viumbe vyote, anayesema katika Kitabu chake Kitakatifu:

{ وَقُلْ اَعْمَلُوا فَسَيَرَى اللّٰهُ عَمَلَكُمْ وَرَسُولُهُ وَالْمُؤْمِنُونَ وَسَتُرَدُّونَ اِلَىٰ عَالَمِ الْغَيْبِ  
وَالشَّهَادَةِ فَيُنَبِّئُكُمْ بِمَا كُنْتُمْ تَعْمَلُونَ }

{Na sema: Tendeni vitendo. Na Mwenyezi Mungu, na Mtume  
wake, na Waumini wataviona vitendo vyenu. Na mtarudishwa kwa  
Mwenye kujua siri na dhaahiri; naye atakuambieni mliyo kuwa  
mkiyatenda.}.

Na ninashuhudia kuwa hakuna Mungu mwingine aabudiwaye kwa  
haki isipokuwa Mwenyezi Mungu Mtukufu, peke yake hana  
mshirika wake. Na ninashuhudia kuwa Bwana wetu na Mtume  
wetu Muhammad ni Mja na Mjumbe wake. Anasema S.A.W: Kama  
Kiama kitasimama na mmoja wenu akawa na mche wa mti  
mkononi mwake, kama ataweza kuupanda basi na afanye hivyo.  
Ewe Mola wetu msalie na umbariki yeye na Jamaa zake na  
Maswahaba wake wote. Na mwenye kuwafuata kwa Wema mpaka  
siku ya Malipo.

Na baada ya utangulizi huu.

Hakika katika Misingi Mikuu ya Uislamu na mafunzo yake mema, ni  
kuipenda nchi, na kuilinda pamoja na kufanya kazi ya kuiendeleza na  
kuifanya isonge mbele zaidi na ni heshima kubwa mno kwa mtu kuwa  
na hisia za Uzalendo wa kweli kwa nchi yake na kufanya juhudi za  
kiutendaji za kuijenga na kuikuza na kuiweka juu zaidi. Kwani Mataifa  
yote yaliyoendelea kiteknolojia na kistaarabu nyuma yake kuna  
wanaume waliosimama kidete kwa kujitolea huku nyoyo zao zikiwa

(۲)

zimejaa Mapenzi kwa nchi zao wakaziimarisha kwa kazi na bidii zenye kuleta matunda kwa watu na nchi. Na nchi yetu ina thamani kubwa sana ya kuyastahiki hayo na zaidi ya hayo, kutoka kwa Watoto wake. Kwani Misri ni moyo hai wa Uarabu na Uislamu, na Misri ni ngao ya Umma na Upanga wake, na ni ngome ya ngome zake katika kupambana na Ugaidi na Changamoto mbalimbali, na kwa ajili hiyo, hakika kuilinda Misri na kufanya kazi ya kuiendeleza na kuiinua ni wajibu wa kidini na wa kitaifa. Misri ni Mlezi wa Ustaarabu na ni taifa la Jumbe za Mwenyezi Mungu Mtukufu, na ni nchi ambayo kutajwa kwake katika Qurani Tukufu kumebatanishwa na Usalama na Amani ambapo anasema Mwenyezi Mungu Mtukufu kupitia Mtume wetu Yusufu A.S:

{ادْخُلُوا مِصْرَ إِن شَاءَ اللَّهُ آمِنِينَ}

.amani na salama kwa Ingieni (:Wataambiwa).

Hapana shaka kwamba Maendeleo na Ujenzi pamoja na kuiinua nchi juu hutoa hakikisho kwa utukufu na heshima ya Umma, na heshima ya watu wake, ambapo ujenzi wa nchi hauwi kwa maneno matupu au kwa ndoto na matarajio bali lazima iwe kwa juhudi pevu na jasho na kwa kujitahidi na kujitolea muhanga na kutumia njia za ujenzi wa maendeleo na sababu za kusonga mbele na Ustaarabu, na miongoni mwa Muhimu katika sababu hizo ni: Mzinduko wa kuzijua changamoto: Kwa kweli Mzinduko wa kuoijua Taifa na kuzijua changamoto zake inazozielekea na aina mbalimbali za hatari zinazolizunguka Taifa ni Jambo linalohitaji kuelewa ukubwa wa changamoto hizo zinazotukabili kwani sisi bila ya kuzitambua vilivyo changamoto hizo na bila ya kuwa na Mzinduko wake hatuwezi kuweka njia za kuzitatua zinazoweza kufanikiwa au zinazofaa kwa changamoto hizo.

Jambo ambalo halina shaka yoyote ndani yake ni kwamba Suala la Mzinduko wa kuijua thamani ya nchi na uhalali wake wa Utaifa na ulazima wa kuunga mkono uendeleaji wake pamoja na kufanya kazi

(3)

ya kuikuza na kuiendeleza ni moja ya misingi muhimu ya Ujenzi wa nchi yenye nguvu, na ni moja ya Nguzo za Uzalendo na Upenzi wa nchi na kwa ajili ya kuzilinda nyenzo zake na kila kitu miongoni mwa Mali zake.

Kama ambavyo Mzinduko wa kuujua umuhimu wa nchi hupelekea kurekebisha mieleweko mibovu ambayo baadhi ya makundi ya kigaidi na yenye Siasa kali yamejaribu kuiimarisha akilini mwao, ambapo makundi hayo yalifanya kazi kubwa ya kuijenga falsafa yake kwa majaribio ya kutaka kuleta mgawanyiko na ukosefu wa kujiamini baina ya Mataifa yote na viongozi wake na wenye majukumu mbalimbali ndani ya Mataifa hayo, ingawa Mafunzo ya Dini zote yanatulingania tuwaheshimu viongozi waadilifu ambapo anasema Mtume wetu S.A.W: Hakika katika kumtukua Mwenyezi Mungu Mtukufu ni kumuheshimu Muislamu mwenye Mvi, na Mwenye kuhifadhi Qurani ambaye hajikwezi ndani yake wala sio mwenye kuachana nayo, na kumuheshimu mwenye madaraka, aliye mwadilifu. Na Mwenyezi Mungu Mtukufu, Msema kweli amemjaalia Mwadilifu siku ya Kiama kuwa katika Watu saba ambao yeye Mtukufu, atawaweka kwenye kivuli cha Arshi yake siku ambayo hakuna kivuli isipokuwa kivuli chake, ambapo anasema S.A.W: (Watu Saba ambao Mwenyezi Mungu Mtukufu atawaweka kwenye Kivuli siku ambayo hapatakuwapo Kivuli chochote kingine isipokuwa Kivuli chake ...) Kisha akamtaja Kiongozi Mwadilifu mwanzoni kabisa mwa Hadithi hii.

Na miongoni mwa Misingi ya Ujenzi wa nchi: Ni kujitolea kwa ajili ya Taifa kwa moyo mmoja sio tu kwa kauli mbiu zinazoonyeshwa au matamshi yanayosemwa, kwani Uzalendo ni mfumo wa Maisha na kuuhi Uhai wa Nchi na changamoto zake zinazoizingira nchi hiyo na kuugua kwa machungu yake pamoja na kufurahia kwa kuyafanikisha matumaini yake na kuwa tayari daima Kujitolea kwa ajili ya Nchi.

Na Ulinzi wa Nchi na Kujitolea kwa ajili yake ni takwa la kisheria na Wajibu wa kitaifa kwa kila anayeishi ndani ya Nchi na ataendelea kuwa chini ya Kivuli chake. Kwa hiyo Kuipenda Nchi hakupatikani kwa

(٤)

kiasi cha hisia za ndani tu bali ni lazima kutafsirike kwa vitendo na kuwa kazi na mwenendo mzuri unaomfaa Mtu na Jamii yake na kwa hivyo, hapana budi kujitolea kwa ajili ya kuendelea kuwapo kwa Nchi yenye nguvu inayopendwa, kwani Uzalendo kwa ajili ya Nchi unawataka Wananchi wake wauazimie na washikane bega kwa bega wote kwa pamoja ili kuulinda. Kwa sababu Utulivu wa Mataifa ni muhimu sana kwa ajili ya kulifikia lengo la Mwenyezi Mungu Mtukufu la kukuumba Mwanadamu ili aujenge Ulimwengu, na kuinyanyua Dini, na kusimamisha Ibada zake. Na Jihadi haikuwekwa kisheria katika Uislamu isipokuwa kwa lengo la kuzilinda Nchi na kurejesha haki za waliodhulumiwa au kushambuliwa. Na kwa sababu hii, Mwenyezi Mungu Mtukufu ameinua juu cheo cha wale wanaojitolea roho zao katika Njia ya Mwenyezi Mungu Mtukufu kwa ajili ya kuzilinda Nchi zao, anasema Mwenyezi Mungu Mtukufu:

{إِنَّ اللَّهَ اشْتَرَى مِنَ الْمُؤْمِنِينَ أَنفُسَهُمْ وَأَمْوَالَهُمْ بِأَنْ لَهُمُ الْجَنَّةَ يُقَاتِلُونَ فِي سَبِيلِ اللَّهِ فَيَقْتُلُونَ وَيُقْتَلُونَ وَعَدًا عَلَيْهِ حَقًّا فِي التَّوْرَةِ وَالْإِنْجِيلِ وَالْقُرْآنِ}.

{Hakika Mwenyezi Mungu amenunua kwa Waumini nafsi zao na mali zao kwa kuwa wao watapata Pepo. Wanapigana katika Njia ya Mwenyezi Mungu - wanauwa na wanauwawa. Hii ni ahadi aliyo jilazimisha kwa Haki katika Taurati na Injili na Qur'ani}.

Na miongoni mwa Mambo na Misingi Muhimu ya Ujenzi wa Mataifa na Staarabu: Ni Ufanisi wa Kazi na Utendaji wa Kweli: Na Uislamu umeinyanyua Thamani ya Kazi na kuifanya kuwa Mlango miongoni mwa Milango ya Ibada, bali ni katika ngazi za juu zaidi za ibada hizo ambapo Mtume S.A.W anasema akiielezea kazi: Kwamba ni Jihadi kwa ajili ya njia ya Mwenyezi Mungu Mtukufu. Kutoka kwa Kaab bin Ajrah R.A amesema kwamba Mtu mmoja alipitia kwa Mtume S.A.W na Maswahaba wake wakaiona ngozi yake na Uchangamfu wake kisha wakasema: Ewe Mtume wa Mwenyezi Mungu, Ingekuwaje kama hali hiyo ingekuwa katika njia ya Mwenyezi Mungu Mtukufu? Mtume S.A.W akasema: Ikiwa Mtum huyo ametoka kwa ajili ya

(٥)

kumuhangaikia mwanae mdogo, basi huyo yuko katika njia ya Mwenyezi Mungu, na ikiwa atatoka kwa ajili ya kuwahangaikia wazazi wake waliozeeka basi yuko katika njia ya Mwenyezi Mungu Mtukufu, na ikiwa ametoka kwa ajili ya kujionesha na kujifakharisha basi mtu huyo yuko katika njia ya Shetani.

Kwa hiyo, Dini na Utaifa au Uzalendo kwa pamoja vinahitaji juhudi kutoka kwetu, jasho, kazi na uzalishaji, na hasa hasa kwa kuwa Dini yetu tukufu ni Dini ya Kazi na Utimizaji wake.

Anasema Mwenyezi Mungu Mtukufu:

{الَّذِي خَلَقَ الْمَوْتَ وَالْحَيَاةَ لِيَبْلُوَكُمْ أَيُّكُمْ أَحْسَنُ عَمَلًا وَهُوَ الْعَزِيزُ الْعَفُورُ }

{Ambaye ameumba mauti na uhai ili kukujaribuni ni nani miongoni mwenu mwenye vitendo vizuri zaidi. Na Yeye ni Mwenye nguvu na Mwenye msamaha}.

Na anasema Mwenyezi Mungu Mtukufu:

{يَا أَيُّهَا الَّذِينَ آمَنُوا إِذَا نُودِيَ لِلصَّلَاةِ مِنْ يَوْمِ الْجُمُعَةِ فَاسْعَوْا إِلَىٰ ذِكْرِ اللَّهِ وَذَرُوا الْبَيْعَ ذَلِكُمْ خَيْرٌ لَكُمْ إِنْ كُنْتُمْ تَعْلَمُونَ \* فَإِذَا قُضِيَتِ الصَّلَاةُ فَانْتَشِرُوا فِي الْأَرْضِ وَابْتَغُوا مِنْ فَضْلِ اللَّهِ وَاذْكُرُوا اللَّهَ كَثِيرًا لَعَلَّكُمْ تُفْلِحُونَ \* وَإِذَا رَأَوْا تِجَارَةً أَوْ لَهْوًا انفَضُوا إِلَيْهَا وَتَرَكُوكَ قَائِمًا قُلْ مَا عِنْدَ اللَّهِ خَيْرٌ مِنَ اللَّهِوِ وَمِنَ التِّجَارَةِ وَاللَّهُ خَيْرُ الرَّازِقِينَ }

{Enyi mlio amini! Ikiadhiniwa Sala siku ya Ijumaa, nendeni upesi kwenye dhikri ya Mwenyezi Mungu, na wacheni biashara. Hayo ni bora kwenu, lau kama mnajua. Na itakapo kwisha Sala, tawanyikeni katika nchi mtafute fadhila za Mwenyezi Mungu, na mkumbukeni Mwenyezi Mungu kwa wingi ili mpate kufanikiwa. Na wanapo iona biashara au pumbao wanayakimbilia hayo na wakakuacha umesimama. Sema: Yaliyoko kwa Mwenyezi Mungu ni bora kuliko pumbao na biashara. Na Mwenyezi Mungu ni Mbora wa watoa riziki}.

(٦)

، ويقول (صلى الله عليه وسلم) : (مَا أَكَلَ أَحَدٌ طَعَامًا قَطُّ خَيْرًا مِنْ أَنْ يَأْكُلَ مِنْ عَمَلٍ يَدِهِ ، وَإِنَّ نَبِيَّ اللَّهِ دَاوُدَ (عَلَيْهِ السَّلَامُ) كَانَ يَأْكُلُ مِنْ عَمَلِ يَدِهِ) .  
على أننا نؤكد أن ديننا الإسلامي لم يطلب منا مجرد العمل إنما طلب منا العمل الجاد المتقن ، حيث يقول الحق سبحانه :

{إِنَّا لَا نُضِيعُ أَجْرَ مَنْ أَحْسَنَ عَمَلًا}

{Hakika wale walio amini na wakatenda mema - hakika Sisi hatupotezi ujira wa anaye tenda mema}.

، ويقول نبينا (صلى الله عليه وسلم) : (إن الله يحب إذا عمل أحدكم عملاً أن يتقنه).  
ومن عوامل بناء الدول والحضارات : العلم ، والإدارة الجيدة :  
فالبناء يحتاج إلى علم وخبرة ودربة وتخصص ، وليس مجرد هواية ، وعندما ننظر في القرآن الكريم والسنة النبوية المطهرة نجد أنهما يؤكدان على ضرورة توفر الكفاءة والكفاية والأمانة، قال تعالى على لسان سيدنا يوسف (عليه السلام) :

{اجْعَلْنِي عَلَى خَزَائِنِ الْأَرْضِ إِنِّي حَفِيظٌ عَلِيمٌ}

{Yusuf akasema: Nifanye mshika khazina za nchi. Kwani hakika mimi ni mlinzi mjuzi.}

وقال جل شأنه على لسان ابنة شعيب في شأن سيدنا موسى (عليه السلام) :

{يَا أَبَتِ اسْتَأْجِرْهُ إِنَّ خَيْرَ مَنْ اسْتَأْجَرْتَ الْقَوِيُّ الْأَمِينُ}

{Akasema mmoja katika wale wanawake: Ewe baba yetu! Muajiri huyu. Hakika mbora wa kumuajiri ni mwenye nguvu na muaminifu}.

(Y)

Na Mtume S.A.W ameonya kuhusu kuwapa madaraka watu wasio kuwa na uwezo na akasema kwamba kufanya hivyo moja ya alama za Kiama akasema Mtume S.A.W: Pindi jukumu linapokabidhiwa kwa wasio na uwezo basi subiri Kiama. Na wasimamizi katika kila Jambo ni wale ambao wana uwezo wa kuongoza na ni waaminifu.

Mtume S.A.W alikuwa akiwapa kazi Maswahaba na Wafanyakazi wake kwa mujibu wa elimu uwezo na utendaji katika majukumu yao, na wala hakuwa akimpa mtu kazi kwa upendeleo au undugu au hata mapenzi. Kutoka kwa Abu Dhar R.A amesema: Nilisema: Ewe Mtume wa Mwenyezi Mungu Mtukufu huwezi kunitumia mimi kikazi? akasema: Mtume S.A.W akampigapiga mabegani kwa mkono wake kisha akasema: Ewe Abu Dhar hakika Wewe ni Dhaifu na kazi hii ni amana, na hakika dhamana ni udhalili na majuto siku ya Kiama, isipokuwa kwa mwenye kuitendea haki yake na akalitekeleza jukumu lake. Na anasema Mtume S.A.W: akimwambia Abdu Rahmani bin Samurah, Ewe Abdu Rahmani: Usimuombe Uongozi, hakika wewe ukipewa kwa kuuomba utapewa jukumu lake, na ukipewa bila ya kuuomba basi utasaidiwa namna ya kuutekeleza.

Na ninaisema kauli yangu hii, na ninamwomba msamaha Mwenyezi Mungu Mtukufu kwa ajili yenu na kwa ajili yangu.

\* \* \*

**Sifa zote njema ni zake mwenyezi Mungu Mtukufu Mlezi wa viumbe vyote. Na rehma na amani ziwe juu ya Mtume wa Mwisho katika Mitume, na Manabii wake Mwenyezi Mungu Mtukufu, Bwana wetu Muhammad S.A.W, na Jamaa zake, na Maswahaba wake wote, na atakayewafuata kwa Wema mpaka siku ya Malipo.**

(A)

Ndugu zangu Waislamu.

Hakika miongoni mwa njia muhimu za kujenga Nchi na Misingi yake ni kuyatanguliza Maadili ya Tabia njema na mienendo , kwani Umma wowote na Staarabu ambazo hazijengwi isipokuwa kwa Maadili na Tabia njema una njia pia za kuuangusha katika asili ya ujenzi wake na sababu za kuinuka kwake.

Hakika ya Tabia njema katika Uislamu zina cheo kikubwa sana kwani Mwislamu huelekea Daraja za juu za Imani kwa Tabia njema hizo, na mizani yake inajipatia uzito siku ya kuoneshwa Matendo yake mbele ya Mwenyezi Mungu Mtukufu ambapo anasema Mtume wetu S.A.W: Hakuna kitu chenye Uzito wa Juu katia Mizani ya Mja Muumini siku ya Kiama kuliko Uzuri wa Tabia zake, na kwamba Mwenyezi Mungu Mtukufu humchukia yule kufanya maovu ya kupindukia.

Na Mtume S.A.W alipoulizwa kuhusu kitu kitakachowaingiza Watu Peponi kwa wingi alisema: Ni kumcha Mwenyezi Mungu Mtukufu na Tabia njema.

الْفَاحِشَ الْبَدِيَّ

Na Mtume S.A.W amezifanya Tabia njema kuwa ndio kigezo cha ukamilifu wa Imani ya mja au Upungufu wake na akasema S.A.W: Muumini mwenye ukamilifu wa imanickatika Waumini, ni Mbora wao wa Tabia njema. Na anasema Mtume S.A.W: Mche Mwenyezi Mungu Mtukufu popote utakapokuwa, na lifuutilizie Jambo ovu kwa jema litakalolifuta, na tangamana na watu kwa Tabia njema.

Kwa hiyo Tabia njema humfanya mwenye nayo awe na maadili mema kama vile Huruma, kuwapendlea Watu wengie heri na kuhangaika katika kuwanufaisha watu na kuleta manufaa kwa Umma katika nchi yake na kwa watu, mbali na Uchoyo na kujipendelea.

Kwani Dini yetu ya Uislamu iliyo tukufu, imesimama kwa msingi wa kuwapendelea wengine na kupenda kuwasaidia, na wala sio kujipendelea na kuwa mchoyo na kuwa na Umimi.

Na miongoni mataifa na Staarabu mbalimbali ni Uadilifu mwamisingi ya Ujenzi wa

(٩)

Na miongoni mwa misingi ya ujenzi wa Mataifa na Staarabu mbalimbali ni Uadilifu, kwani nchi hujengwa kwa Uadilifu unaowaweka sawa watu wote katia haki na wajibu wa kila mmoja wao, bila ya kumpambanua yoyote na mwingine na jambo hili ni amri ya Mwenyezi Mungu Mtukufu katika kitabu chake ambapo anasema:

{إِنَّ اللَّهَ يَأْمُرُ بِالْعَدْلِ وَالْإِحْسَانِ وَإِيتَاءِ ذِي الْقُرْبَىٰ وَيَنْهَىٰ عَنِ الْفَحْشَاءِ وَالْمُنْكَرِ  
وَالْبَغْيِ يَعِظُكُمْ لَعَلَّكُمْ تَذَكَّرُونَ}

{Hakika Mwenyezi Mungu anaamrisha kufanya uadilifu, na hisani, na kuwapa jamaa; na anakataza uchafu, na uovu, na dhulma. Anakuwaidhini ili mpate kukumbuka}.

Na Hakika wamesema kwamba Mwenyezi Mungu Mtukufu anainusuru nchi yenye Uadilifu hata kama ni ya kikafiri na wala hainusuru nchi yenye Dhuluma hata kama itakuwa ni ya kiislamu kwani kama nchi hiyo ingekuwa ya Kiislamu kweli kweli isingelikubali kuridhia dhuluma itendeke au isingekuwapo Dhuluma hiyo na kwa hivyo wakasema: Hakika nchi zinaweza kudumu kwa ukafiri na uadilifu na wala hazidumu kwa Uislamu na dhuluma; kwa kuwa kufuata kwake Dini kwa Wakati huo kutakuwa ni ufuasi wa juu juu tu hakumaanishi mweleweko kamili wa Uislamu wala madhumuni yake ya juu ambayo yanajengeka kwa Haki na Uadilifu na kuikana Dhuluma na Uonevu wa aina zake zote na maumbile yake.

Ewe Mwenyezi Mungu wetu Mtukufu tunakuomba uzipe nchi zetu Usalama na Uwawafikishe viongozi wetu na wasimamizi wote wa Mambo yetu, zilinde nchi zetu kutokana na vitimbi vya Watu wenye kufanya vitimbi hivyo, na Ufisadi wa Mafisadi. Na Dua yetu ya mwisho ni Alhamdulillah Rabi Alaalameen.

(10)